



## TANGAZO KWA UMMA

### KUHUSU BENKI ZA TANZANIA WOMEN'S BANK PLC, TANDAHIMBA COMMUNITY BANK LTD NA KILIMANJARO COOPERATIVE BANK LTD

Itakumbukwa kuwa mnamo tarehe 4 Januari 2018, Benki Kuu ya Tanzania iliziongezea benki za Tanzania Women's Bank Plc (TWB), Tandahimba Community Bank Limited (TACOBA) na Kilimanjaro Cooperative Bank Limited (KCBL) muda wa miezi sita mpaka tarehe 30 Juni 2018 ili kuweza kutimiza vigezo vya mtaji kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake. Aidha benki hizo ziliongezewa muda wa mwezi mmoja hadi tarehe 31 Julai 2018 ili kukamilisha taratibu za kuongeza mtaji.

Sambamba na mkakati wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kurekebisha na kuboresha muundo wa benki za umma, wanahisa wa TWB and TPB wameamua kuunganisha benki hizi ili kuboresha ufanisi na utendaji wa benki hizo. Kufuatia muungano huo, kutakuwepo na benki moja ambayo itaendelea kuitwa benki ya "TPB Bank Plc".

Kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 30(1)(a) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Benki Kuu ya Tanzania imeridhia ombi la uunganishaji wa benki za TWB na TPB na kuwa benki moja kuanzia tarehe **03 Agosti 2018** itakayoendelea kuitwa benki ya "TPB Bank Plc" ambayo itaendelea kuwa na mtaji wa kutosha kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 17 cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006. Hivyo, wateja, wafanyakazi, mali na madeni yote ya benki ya TWB yataunganishwa na yale ya benki ya TPB.

Aidha, umma unataarifiwa kuwa benki za TACOBA na KCBL kwa sasa zimeweza kuongeza mtaji na kukidhi kiwango kinachohitajika kisheria na hivyo zinaendelea na shughuli zake kama kawaida.

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuuhakikishia umma kuwa itaendelea kulinda maslahi ya wenyewe amana katika mabenki kwa lengo la kuleta uhimilivu katika sekta ya fedha.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na Mkurugenzi, Kurugenzi ya Usimamizi wa Mabenki, Benki Kuu ya Tanzania, simu namba +255 22 2235483, nukushi +255 22 2234189 au barua pepe - [dbs@bot.go.tz](mailto:dbs@bot.go.tz).

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**02 August 2018**